TANGAZO LA SERIKALI Na. 511 la tarehe 14/9/2018

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

---

# SHERIA NDOGO

---

*(Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kondoa

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

*"Ada na Ushuru"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au Wakala wake kwa ajili ya Huduma, Vibali au Leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Umma aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

*"Bidhaa"* maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa.

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kondoa.

*"Kibali"* maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

*"Machinjio"* maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na

kuanika ngozi.

*"Madini ya Ujenzi"* maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Kifusi, Udongo Mfinyanzi au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za Ujenzi.

*"Maegesho"* maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

*"Magulio, Masoko na Minada"* maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

*"Mali za Halmashauri"* ni pamoja nyumba za Halmashauri, ukumbi wa Halmashauri na Magari ya Halmashauri,Mitambo na Vibanda vya Halmashauri.

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri anayekaimu nafasi ya Mkurugenzi kwa wakati huo

*"Wakala"* maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na ushuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha 4(1) cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika Vyanzo vifuatavyo:-

(a) Ushuru wa kukodisha Mali za Halmashauri

(b) Ushuru wa Madini na Ujenzi

(c) Ushuru wa Minada

(d) Ushuru wa Masoko

(e) Ushuru wa Magulio

(f) Ushuru wa stendi, Maegesho na Ada ya Usajili wa vyombo vya usafiri

(g) Ushuru wa Mazao ya Kilimo

(i) Ushuru wa Mifugo.

(k) Ada ya Usajili Vikundi

(m) Ushuru wa Huduma za Vyoo vya Umma

(n) Ada ya Vibali vya biashara na Leseni ya vileo

(o) Ada ya Vibanda vya Biashara vya Halmashauri

(p) Ada ya Ukaguzi wa Afya

(q) Ada ya Uzoaji taka

(r) Ada ya Vibali vya Ujenzi

Namna ya kukusanya Ada na Ushuru

5. (1) Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 4(2) cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielekitroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(3) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni, au kibali.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(2) cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au Wakala kwa idhini ya Mkurugenzi atatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika endapo stakabadhi ya kielekitroniki haiwezi kutolewa.

(5) Halmashauri au Wakala atakua na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au Wakala haitalipiwa Ada au Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika

haraka, Halmashauri itakua na mamlaka ya kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatikana zitawekwa kwenye akaunti ya Halmashauri.

(7) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru

6 (1) Ni wajibu kwa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa Mfanyabiashara au mtu yeyote kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila Mfanyabiashara au mtu yeyote anaetaka kufanya biashara au jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Uteuzi wa wakala

8. Halmashauri itakua na mamlaka ya kuteua kampuni au taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya na kupokea Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango

kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) kukusanya Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

10. Itakua ni kosa kwa wakala endapo:-

(a) atajaribu au atakusanya Ushuru bila idhini ya Halmashauri;
(b) atajaribu au atakusanya Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoidhinishwa na Sheria Ndogo hizi;
(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ushuru kilichokubaliwa katika Mkataba wa kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(d) atashindwa kutoa stakabadhi halali ya malipo ya Ushuru aliokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo au jengo lolote kwa nia ya kukusanya, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusiana na Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia

12 Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yeyote kwa uzembe au makusudi wakati wa kukusanya Ada na Ushuru au wakati anatekeleza Sheria Ndogo za Halmashauri.

Makosa

13. Itakua ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote;-

(a) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru;
(b) atashindwa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
(c) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(d) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(e) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.
(f) atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(g) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Kufifilisha makosa

14. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (Tshs. 500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama itakavyoelekezwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

15. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) jela na kisichozidi miaka miwili (2) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 4(1)*

### SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa kukodisha mali za Halmashauri

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 2. | Magari ya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 3. | Ukumbi wa Halmashauri | Tsh.200,000/= |
| 4. | Vibanda vya biashara (kwa mwezi) | Tsh.30,000/= |
| 5. | Mitambo ( trekta, vifaaa vya GPS) | Kwa mujibu wa mkataba |

### SEHEMU YA PILI

Ushuru wa Madini ya Ujenzi

| Na. | Aina ya Chanzo | Ukubwa wa Mzigo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|---|
| 1. | Kokoto, Mchanga na Mawe | Tani 1 hadi tani 3 | Tsh.3000/= kwa safari |
| 2. | Kokoto, Mchanga na Mawe | Tani 3 hadi tani 7 | Tsh.5000/= kwa safari |
| 3. | Kokoto, Mchanga na Mawe | Kila tani inayoongezeka | Tsh.1000/= kwa safari |

## SEHEMU YA TATU

Ushuru wa Minada

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh.5000 |
| 2. | Mbuzi | Tsh.1500 |
| 3. | Kondoo | Tsh.1500 |

## SEHEMU YA NNE

Ushuru wa Masoko

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Vibanda vya sokoni | Tsh.1000/= |
| 2. | Meza za Sokoni | Tsh.500/= |
| 3. | Meza za chini | Tsh.500/= |
| 4. | Choo cha sokoni | Tsh.200/= |
| 5. | Kizimba cha Mitumba | Tsh.500/= |

## SEHEMU YA TANO

Ushuru wa Magulio

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Meza za chini | Tsh.200/= |
| 2. | Biashara za promotion kwa siku (Binafsi) | Tsh.10,000/= |
| 3. | Biashara za promotion kwa siku (Makampuni) | Tsh.30,000/= |

SEHEMU YA SITA

Ushuru wa stendi, Maegesho na Ada ya Usajili wa vyombo vya usafiri

(a) Ushuru wa Stendi

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Magari Makubwa (kwa siku) | Tsh.2000/= |
| 2. | Mabasi ya kati | Tsh.1000/= |
| 3. | Magari binafsi | Tsh.500/= |
| 4. | Bajaji au Pikipiki | Tsh.200/= |
| 5. | Mikokoteni | Tsh.100/= |

(b) Ushuru wa maegesho kwa maeneo yaliyotengwa

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki iliyosajiliwa kwa biashara katika maeneo yaliyotengwa | Tsh 300/=kwa siku |
| 2. | Teksi | Tsh 500/=kwa siku |
| 3. | Lori chini ya tani 7 au pick up au basi dogo | Tsh 500/=kwa siku |
| 4. | Lori zaidi ya tani 7 au basi kubwa | Tsh 1,000/=kwa siku |
| 5. | Magari mengine yasiyo ya biashara | Tsh 200/=kwa saa<br>Tsh 500/=kwa siku |
| 7. | Gharama za kukokota gari lililotelekezwa | Tsh 30,000/= |

Ada ya ushuru wa kusajili vyombo vya usafiri

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki za biashara | Tsh 10,000/= |
| 2 | Taksi au pick up | Tsh 15,000/= |
| 3 | Gari ya abiria chini ya 25 | Tsh 20,000/= |
| 4 | Gari za abiria Zaidi ya 25 na malori yanayoegeshwa maeneo ya halimashauri | Tsh 30,000/= |

SEHEMU YA SABA
Ushuru wa Mazao ya Kilimo

| Na. | Aina ya Chanzo | Kipimo kwa KGS | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|---|
| 1. | Alizeti | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 2. | Karanga | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 3. | Mahindi | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 4. | Mtama | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 5. | Maharage | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 6. | Kunde | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 7. | Ulezi | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 8. | Vitunguu | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 9. | Nyonyo | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 10. | Choroko | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 11. | Dengu | Gunia la Kg 100 | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |

SEHEMU YA NANE

Ushuru wa Mifugo

(a) Ushuru wa Machinjio

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh. 10000/= kwa kila ng'ombe atakayechinjwa |
| | Mbuzi | Tsh. 2500/= kwa kila mbuzi atakayechinjwa |
| 2. | Kondoo | Tsh. 2500/= kwa kila kondoo atakayechinjwa |
| 3. | Nguruwe | Tsh. 2500/= kwa kila nguruwe atakayechinjwa |
| 4. | Ngozi Ng'ombe | Tsh.400/= kwa kila kipande cha ngozi ya ng'ombe |
| 5. | Ngozi mbuzi | Tsh 250/=kwa kila kipande cha ngozi ya mbuzi au kondoo |

(b) Ada ya ukaguzi wa nyama Minadani

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh 3000/= |
| 2. | Mbuzi | Tsh. 500 |
| 3. | Kondoo | Tsh. 500 |

(c) Vibali vya kuuza Mifugo Minadani

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh. 2000/= |
| 2. | Mbuzi | Sh. 1000/= |
| 3. | Kondoo | Sh. 1000/= |

SEHEMU YA TISA

Ada ya Usajili wa Vikundi

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Vikundi (kwa mwaka) | Sh. 15,000/= |

SEHEMU YA KUMI

Ushuru wa Huduma ya Vyoo vya Umma

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Choo cha Stendi | Tsh. 200 |
| 2. | Choo cha Sokoni | Tsh. 200 |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Ada ya Vibali vya biashara na Leseni ya vileo.

| Na. | Aina ya Chanzo | Muda | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha biashara | Miezi sita | Tsh.50,000/= |
| 2 | Bar | Miezi sita | Tsh.30,000/= |
| 3 | Glosari | Miezi sita | Tsh.40,000/= |
| 4 | Pombe za kienyeji | Miezi sita | Tsh.12,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ushuru wa Vibanda vya Halmashauri

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Vibanda vizungukavyo sokoni – kwa mwezi | Tsh.50,000/= |
| 2 | Vibanda vizungukavyo stendi – kwa mwezi | Tsh.50,000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ada ya Ukaguzi wa Afya

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Kupima Afya | Tsh 5000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA NNE

A: ADA ZA KUZOLEA TAKATAKA

| Na. | AINA YA BIASHARA | ADA KWA MWEZI | ADA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Vilabu vya pombe za kienyeji | Tsh.1,000/= | Tsh.12,000/= |
| 2. | Maduka ya rejarejaaa/jumla | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/ |
| 3. | Mama, Baba lishe | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 4. | Ghala za mbao | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 5. | Restaurant au hotel | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 6. | Maduka ya jumla | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 7. | Nyumba za kulala wageni | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 8. | Mashine za kusaga na kukoboa nafaka | Tsh.4,000/= | Tsh.48,000/= |
| 9. | Viwanda vya mikate | Tsh.3,000/= | Tsh.36,000/= |
| 10. | Mashine za kuranda mbao | Tsh.4,000/= | Tsh.48,000/= |
| 11. | Ofisi mbalimbali | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 12. | Bar au grocery | Tsh.5000/= | Tsh.60,000/= |
| 13. | Viwanda vya uselemara | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 14. | Saloon au vinyozi | Tsh.2,000/= | Tsh.24,000/= |
| 15. | Gereji | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 16. | Kuchoma mahindi | Tsh.5,00/= | Tsh.6,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17. | Kuuza barafu | Tsh.500/= | Tsh.6,000/= |
| 18. | Maduka ya nyama | Tsh.3,000/= | Tsh.36,000/= |
| 19. | Maduka ya kuchomelea au workshop welding | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 20. | Biashara zote ndogondogo | Tsh.500/= | Tsh.6,000/= |
| 21. | Wauzaji mkaa jumla | Tsh.3,000/= | Tsh.36,000/= |
| 22. | Vituo vya kujazia mafuta | Tsh.10,000/= | 120,000/= |
| 23. | Zahanati binafsi | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 24. | Hospital au vituo vya Afya binafsi | Tsh.10,000/= | Tsh.120,000/= |
| 25. | Ghala | Tsh.10,000/= | Tsh.120,000/= |
| 26. | Viwanda vya kukamua mafuta | Tsh.10,000/= | Tsh.120,000/= |
| 27. | Shule au Vyuo binafsi | Tsh.5,000/= | Tsh.60,000/= |
| 28. | Mafundi cherehani | Tsh.1,000/= | Tsh.12,000/= |
| 30. | Vizimba sokoni(kila kimoja) | Tsh.100/= | Tsh,1,200/= |

B: MAKAMPUNI

| Na. | JINA LA KAMPUNI/TAASISI | ADA KWA MWEZI | ADA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1. | NMB | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |
| 2. | CRDB | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |
| 3. | POSTAL | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |
| 4. | TTCL | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |
| 5. | TANESCO | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |
| 6. | MAKAMPUNI MENGINE | Tsh.30,000/= | Tsh.360,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TANO

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

Ada ya Huduma ya Ardhi

| Na. | Aina ya Chanzo | Aina ya matumizi | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kiwanja | | Tsh.20,000/= |
| 2. | Maombi ya kupimiwa shamba au kiwanja | | Tsh.80,000/= |
| 3. | Ada ya kibali cha Ujenzi | | Tsh. 20,000/= |
| 4. | Ukaguzi wa ramani ya jingo | (a) Matumizi ya makazi | Tsh. 20,00/= |
| | | (b) Matumizi ya biashara na makazi | Tsh. 40,000/= |
| | | (c) Matumizi ya biashara | Tsh. 60,000/= |
| | | (d) Matumizi ya kiwanda | Tsh. 100,000/= |
| | | (e) Jengo linalofanyiwa ukarabati tofauti na awali | 50% ya Ada ya awali |
| | | (f) Jengo linalofanyiwa upanuzi | 50% ya Ada ya awali |
| | | (g) Jengo linalofanyiwa upanuzi na ukarabati kwa pamoja | 100% ya Ada ya awali |

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 14)*

Mimi ........................................................................................ nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya........................................................ ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa kwamba mnamo tarehe .........ya mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe .....................ya Mwezi ..............................Mwaka ……

Jina: ..................................................

Saini: ..................................................

Mbele ya: ..........................................

Cheo: ................................................

Saini: ................................................

Tarehe: ............................................

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

KHALIFA KONDO
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S

HAMZA MAFITA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI,

DODOMA,
15 Agosti, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*